**Kumb. Na. AB.16/194/02/VOL.II/122** **Tarehe: 13/02/2024.**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema anawatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapo chini. Hii ni baada ya kupokea Kibali cha Ajira chenye **Kumb. Na. FA.228/613/01"A" /006** cha tarehe **02 Januari, 2024** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

## MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III – NAFASI (02)

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha Nne (IV) au kidato cha sita (VI)
- Awe amehitimu Mafunzo ya Astashahada katika moja ya fani zifuatazo: - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma au kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i) Mtendaji Mshauri wa Halmashauri ya Kijiji na Kamati zake katika Mipango ya maendeleo ya kijamii na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo
ii) Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na Matumizi ya Serikali ya Kijiji
iii) Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji
iv) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji
v) Katibu wa Kamati ya Halmashauri ya Kijiji
vi) Kutafsiri sera, utaratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogondogo za Halmashauri ya Kijiji
vii) Kuratibu na kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika Kijiji chake na kuziwasilisha katika Kata
viii) Kuongoza vikao vya maendeleo ya Kijiji vinavyohusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake
ix) Kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa, umasikini na Uzalishaji
x) Kusimamia matumizi bora ya nguvu kazi
xi) Kiongozi wa wakuu wa vitengo wa kitaalamu katika Kijiji

### 1.3: MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Serikali TGS B

## 2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI (01)

### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe Amehitimu Elimu ya kidato cha Nne (IV) au kidato cha sita (VI)
- Awe amehitimu mafunzo ya Stashahada/cheti **NTA LEVEL 6** katika mojawapo ya fani ya Utunzaji wa Kumbukumbu kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 2.2MAJUKUMU YA KAZI

i. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na kuyapeleka kwa Maafisa husika
ii. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
iv. Kuweka/ kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (file racks/cabinets) katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
v. Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka n.k) katika mafaili.
vi. Kushughulikia maombi ya Kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.
vii. Kufuatilia mzunguko wa Majalada ndani ya Taasisi

### 1.3: MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Serikali TGS C

### MASHARTI KWA UJUMLA.

i) Mwombaji anatakiwa awe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
ii) Mwombaji aambatishe cheti cha kuzaliwa
iii) Mwombaji ambaye tayari ni Mtumishi wa Umma na amejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na alizonazo, apitishe barua yake ya maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wake.
iv) Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
v) Maombi yote yaambatishwe na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya Kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
    - ✓ Certificates
    - ✓ Diploma
    - ✓ Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI
    - ✓ Computer Certificate
    - ✓ Vyeti vya kitaaluma (Professional certificate from respective boards)
    - ✓ Picha moja “Passport size” ya hivi karibuni.
vi) Testmonial, **“Provisional Results”, “Statement of Results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) *HAVITAKUBALIWA***
vii) Mwombaji aliyesoma nje ya Tanzania ahakikishe vyeti vyake vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).

viii) Mwombaji wa nafasi ya Ajira aliyestaafishwa/kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma haruhusiwi kuomba isipokuwa kama anakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

ix) Mwombaji wa kazi ambaye tayari ni mwajiriwa katika nafasi ya kuingilia aliyeko katika Utumishi wa Umma asiombe kwa kuzingati maelekezo yaliyo katika **Waraka Na. CAC. 45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba ,2010**.

***x) Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachuliwa hatua za kisheria.***

**xi)** Maombi yote yaombwe kwenye Mfumo wa Kielekitroniki wa Ajira (*R**ecruitment portal***) kupitia anuani ifuatayo: - **http://portal.ajira.go.tz** (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ***Recruitment portal*)**

xii) Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu (kwa njia ya Posta/Mkono) na kwa kutofuata utaratibu uliobainishwa katika tangazo hili **Hayatapokelewa.**

xiii) Kumbuka Kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi katika Mfumo iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu vilivyothibitishwa na Mwanasheria, Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa: -

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA**
**S.L.P 175**
**SENGEREMA**

xiv) Mwisho wa kupokea maombi ya kazi katika mfumo ni tarehe **26 Februari, 2024**.

Tangazo hili limetolewa na: -

Binuru M. Shekidele.
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**SENGEREMA.**